Afya ya wanawake



Wanawake wenye vijidudu vya ukimwi

Dalili gani huwasumbua wanawake wenye vijidudu vya ukimwi?

Wanawake wenye maambukizi ya vijidudu vya ukimwi hupitia dalili nyingi ambazo wanaume wenye vidudu vya ukimwi huwa nazo. Hata hivyo, kuna kujisikia kwa aina fulani kunakoambatana na dalili za HIV/AIDS ambazo huwatokea wanawake tu. Hizi zinaweza kuwa kama shida za wakati wanawake wakiwa kwenye hedhi, mambukizi kwenye sehemu za ukeni (cervical dysplasia) na kansa ya tumbo la uzazi.

Wanawake pia huweza pitia maradhi tofauti yatokanayo na madawa ya kupigana na vijidudu vya ukimwi kuliko wanaume. Vile vile, kuna shida zaidi wakati wa ujauzito na malezi ya mtoto kwa wanawake wenye maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.

Matatizo ya Hedhi

- Wanawake wenye maambukizi ya vijidudu vya ukimwi huweza kukabiliwa na mabadiliko katika kuona damu wakati wa hedhi. Wanawake hawa wanaweza kuanza kupata mizinguko isiyo ya kawaida, kutokwa damu kwa wingi au kidogo, au wanaweza kutoona kabisa damu za hedhi.
- Vilevile, wanawake wenye vijidudu vya ukimwi mara kwa mara hukabiliwa na maumivu makali kabla ya mwandamo wa hedhi. (Premenstrual syndrome).

Mabadiliko haya yanaweza kuhusishwa au kutohusishwa moja kwa moja na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi. Sababu nyingine nyingi, kama vile msongo wa mawazo wa muda mrefu, kupunguwa kwa uzito wa mwili, matumizi ya pombe na dawa za kulevya kwa muda mrefu, ujauzito, na magonjwa mengine ya muda mrefu ama matumizi ya matibabu fulani yanaweza

Canadian AIDS Treatment Information Exchange
Réseau canadien d'info-traitements sida
www.catie.ca

www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

pia yakasababisha mabadiliko katika mwandamo wa hedhi. Kama una baadhi ya matatizo yaliyotajwa hapo juu, ni vizuri daktari wako au mtaalamu wa akina mama ayachunguze

Maambukizi ya sehemu za ukeni

Maambukizi ya sehemu za ukeni, hususani utando, ni ya kawaida kwa wanawake wenye vijidudu vya ukimwi. Kwa kuwa na mfumo wa kupingana na magonjwa uliopuguwa nguvu, baadhi ya maambukizi haya huja na kupona, na kurudia tena mara kwa mara hivyo yanahitaji matibabu makali kuliko ilivyo kawaida.

Uvimbe Usio wa Kawaida Katika Nyonga (Cervical dysphasia)

Uvimbe usio wa kawaida katika nyonga (Cervical dysphasia), au mabadiliko katika chembechembe za mfuko wa uzazi, hutokea zaidi kwa wanawake wenye vijidudu vya ukimwi kuliko wale wasionavyo. Hii ni dalili ya kupatwa na saratani, na isipotibiwa, huweza kuendela kuwa saratani ya mfuko wa uzazi. Kwa bahati nzuri, uvimbe usio wa kawaida katika nyonga na saratani ya mfuko wa uzazi vinazuilika. Kufanya vipimo vya Pap Smears ili kuchunguza dalili hizi kunawezesha kupata matibabu mapema.

Madhara Yaletwayo na Dawa za Kutibu Vijidudu vya Ukimwi

Utumiaji mzuri wa mchanganyiko wa madawa wa kupigana na vijidudu vya ukimwi kunaweza kukusaidia kupunguza wingi wa vijidudu mwilini mwako na kuinua uwezo wako wa kupigana na maambukizi kwa kutia nguvu mpya katika mfumo wako wa kukinga magonjwa. Hii pia husaidia katika kupunguza hatari za kupatwa na maambukizi na dalili nyingine ziendanazo na vijidudu vya ukimwi, pamoja na matatizo hedhi, kurudiwa na maambukizi ya ute ukeni na uvimbe usio wa kawaida katika nyonga.

Kwa upande mwingine, wanawake huweza kupatwa na madhara tofauti kutokana na matumizi ya madawa ya kupigana na ukimwi ukiwalinganisha na wanaume.Hii yaweza kusababisha wanawake kupewa viwango tofauti vya matumizi ya dawa hizi. Kwa baadhi ya wanawake wanaotumia dawa za kuzuia vijidudu vya ukimwi visizaliane mwilini (protease inhibitors) wanaweza kuona mabadiliko ya maumbile ya miili yao, zaidi kuongezeka kwa ukubwa wa matiti na kiuno. Vile vile, baadhi ya dawa za kupigana na vijidudu vya ukimwi zaweza kusababisha kutofanya kazi vizuri kwa dawa za uzazi wa mpango. Hakikisha unaongea na daktari wako juu ya madhara ya dawa zote unazoshauriwa na wataalamu kutumia; na dawa zote unazoweza

kutumia bila kuambiwa na wataalamu, kama vile dawa za uzazi wa mapango, dawa za kuongeza virutubisho mwilini na dawa za miti shamba (herbs).

Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Ujauzito

Kuwa na jividudu vya ukimwi mwilini hakumaanishi kuwa huwezi kuwa na watoto. Vile vile haimaanishi kuwa lazima mtoto wako atakuwa na vijidudu vya ukimwi. Kuna matibabu yanayotolewa wakati wa ujauzito na/ama wakati wa kujifungua ambayo husaidia kupunguza hatari ya mtoto wako kuambukizwavijidudu vya ukimwi. Tafadhali hakikisha unaonana na daktari au mkunga wako ili kujadili juu ya matibabu haya wakati wowote.

Vijidudu vya ukimwi huweza kuambukizwa kwa mtoto kwa kumnyonyesha mtoto maziwa yako, wanawake wenye vijidudu vya ukimwi hawashauriwi sana kuwanyonyesha watoto wao.

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu ya afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

ACAS Asian Community AIDS Services
www.acas.org

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem

GlaxoSmithKline

Shire BioChem